Kikosi Maalumu cha Jeshi la Marekani katika Afrika
Ofisi ya Maswala ya Umma

Wasifu

Jenerali William E. "Kip" Ward

Kamanda, Kikosi Maalumu cha Jeshi la Marekani katika Afrika

Jenarali William E. (Kip) Ward alikuwa kamanda wa kwanza wa Kikosi Maalumu cha Jeshi la Marekani katika Afrika mjini Stuttgart, Ujerumani, Oktoba 1, 2007. Kikosi Maalumu cha Jeshi la Marekani katika Afrika ni moja ya vikosi sita vilivyounganishwa kijografia ndani ya Wizara ya Ulinzi ya Marekani katika mfumo mmoja wa utawala.

Jenarali Ward alihitimu mafunzo na kuingizwa rasmi katika jeshi la kikosi cha askari wa miguu mwezi June mwaka 1971. Elimu yake ya kijeshi ni pamoja na mafunzo ya awali na ya juu ya maafisa wa jeshi la kikosi cha askari wa miguu, ukomanda katika jeshi la ardhini la Marekani na mafunzo katika chuo cha majenarali, na chuo cha Marekani cha Mambo ya Vita. Ana shahada ya pili (MA) katika Sayansi ya Siasa kutoka chuo kikuu cha Pennsylvania na shahada ya kwanza katika Sayansi ya Siasa kutoka chuo kikuu cha Morgan cha jimbo. Utumishi wake katika jeshi ni pamoja na kazi ambayo aliifanya nchini Korea, Misri, Somalia, Bosnia, Israeli, pia nchini Ujerumani ambako alifanya kazi safari mbili, na kazi mbali mbali katika maeneo mbali mbali ya Marekani pamoja nayo jimbo la Alaska na Hawaii.

Utawala wake na kazi zake jeshini ni pamoja na kuwa Kiongozi wa Platuni, Batalioni ya tatu ya vikosi vya angani, kikosi cha majeshi ya miguu cha 325, Kikosi cha 82 cha askari wa angani, Kambi ya Fort Bragg, North Carolina; Kamanda wa kikosi cha bunduki , Batalioni ya Kwanza (yenye vifaru), kikosi cha 17 cha wanajeshi wa miguu, kikosi cha 2 divisheni ya jeshi la miguu, Kambi ya Howze, nchini Korea; Kikosi cha ugavi na usafirishaji wa watu na vitu S-4, Brigedi ya 210 ya kikosi cha mizinga, Vikosi vya VII, Jeshi la Marekani katika Ulaya na Jeshi la Saba, Ujerumani; Afisa Mwandamizi, Bataliani ya kwanza (Yenye vifaru), Kikosi cha 7, divisheni ya tatu ya vikosi vya miguu, Jeshi la

Marekani katika Ulaya na Jeshi la Saba, Ujerumani; Kamanda, Bataliani ya 5, kikosi cha 9, Brigedi ya 2, baadaye kikosi cha G-4 (ugavi na usafirishaji wa watu na vitu), Divisheni ya 6 ya kikosi cha wanajeshi wa miguu (silaha nyepesi), Kambi ya Fort Wainwright, Alaska; Kamanda, Brigedi ya 2, Divisheni ya 10 ya Milima (silaha nyepesi), Kambi ya Drum, New York na Operesheni Rejesha Matumaini, Mogadishu, Somalia; Kamanda Msaidizi wa Divisheni (Uungaji mkono), Divisheni ya 82 jeshi la angani, Kambi ya Fort Bragg, North Carolina; Jenarali Mtawala wa divisheni ya 25 ya jeshi la miguu (Silaha nyepesi) na Jeshi la ardhini la Marekani, Hawaii, Kambi ya Schofield, Hawaii; na Kamanda, kikosi cha Usawazishaji, Operesheni Ongoza Pamoja, Sarajevo, Bosnia.

Nyadhifa zake za kiutumishi jeshini ni pamoja na: Ofisa Mwandamizi, Jeshi la Ardhini la Marekani linaloshughulikia mambo ya jamii – Aschaffenburg, Jeshi la Marekani katika Ulaya na Kikosi cha Saba, Ujerumani; Ofisa wa Jeshi (Kikosi cha Ugavi na Usafirishaji wa watu na vitu), Ofisi ya Naibu Mkuu wa Utawala wa Mambo ya Ugavi, Jeshi la Marekani, Washington, DC; Ofisa Mwandamizi kwa Makamu Mkuu wa Utawala, Jeshi la Marekani, Washington, DC; Naibu Mkurugenzi wa Operesheni za kijeshi, kikosi J-3, Makao ya Kijeshi ya Taifa, Utawala wa Pamoja wa Jeshi, Washington, DC; Mkuu, Ofisi ya Ushirikiano wa Kijeshi, Misri, Ubalozi wa Marekani, Misri; na Makamu Mkurugenzi wa Operesheni, J-3, Utawala wa Pamoja wa Jeshi la Marekani, Washington, DC.

Kabla ya kushika wadhifa wake wa sasa, Ward alikuwa Naibu Kamanda, Makao Makuu ya Jeshi la Marekani katika Ulaya, Stuttgart, Ujerumani. Huko nyuma alitumika kama Naibu Kamanda Mkuu/ Mkuu wa majeshi, Jeshi la Marekani katika Ulaya na katika Kikosi cha Saba cha Jeshi. Akiwa katika wadhifa wake huu, alichaguliwa na Waziri wa Mambo ya Nchi za Nje wa Marekani kutumika kama Mratibu wa Maswala ya Ulinzi wa Marekani, katika Mamlaka ya Israeli na Palestina ambako alitumika kuanzia mwezi Machi hadi Desemba 2005.

Tunzo na tepe ambazo ametunukiwa Jenarali Ward ni pamoja na nishani ya Utumishi Bora (ikiwa na kishada cha Jani la Mwaloni); Nishani ya kawaida ya Utumishi Bora; Nishani ya Ustahili wa Hali ya Juu ya Ulinzi (Vishada viwili vya Jani la Mwaloni); Nishani ya Ustahili (vishada vitatu vya Jani la Mwaloni); Nishani ya Ulinzi kwa mwanajeshi mwenye kutunukwa; Nishani ya kutunukwa (yenye Vishada sita vya Jani la Mwaloni); Nishani ya Sifa Jeshi la Utawala wa Pamoja; Nishani ya sifa ya Jeshi la Ardhini (yenye Vishada vitatu vya Jani la Mwaloni); Nishani ya kufanikisha ya Jeshi la Ardhini (yenye kishada cha Jani la Mwaloni); tepe ya mwanajeshi mtaalamu wa jeshi la miguu; Tepe ya Ustadi katika Mapigano; na tepe ya ustadi katika kuruka na mwamvuli angani.

Kikosi Maalum cha Jeshi la Marekani katika Afrika ▪ Masuala ya umma na Shughuli za kimataifa za kutoa huduma kwa jamii
+49 (0) 711-729-4714 / 4711 (Stuttgart, Germany)
PublicOutreach@africom.mil
www.africom.mil